Tangazo la Serikali Na. 266 la tarehe 15/06/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(Sura ya 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA KITUO CHA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO) ZA HALMASHAURI YA MJI KIBAHA, 2018

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Mji Kibaha za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kibaha.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

*"Ushuru"* maana yake ni tozo au malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

*"Afisa Mwidhiniwa"* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

*"Gari"* maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu au watu na mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine ambacho kina leseni ya kufanya shughuli hiyo.

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Mji Kibaha.

*"Kituo cha Magari"* maana yake ni eneo lolote ndani ya Halmashauri lililotengwa kwa madhumuni ya kupakia au kushusha abiria na mizigo ikijumuisha maeneo ya minada na masoko ambayo yametengwa kwa ajili ya magari kupakia na kushusha abiria na mizigo.

*"Mabasi"* maana yake ni magari ya abiria yanayofanya safari zake ndani na nje ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha ikijumuisha "Coaster" na "Hiace".

*"Maegesho"* maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha magari.

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha na Afisa yeyote atakayekuwa anafanya kazi za Mkurugenzi kwa wakati huo.

*"Wakala"* maana yake ni mtu yeyote, shirika, kampuni, taasisi au asasi iliyoingia mkataba na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

Mabasi kuingia kituoni

4. Mabasi yote yanayotoka na kwenda mikoani na maeneo mengine ndani ya Halmashauri pamoja na magari ya mizigo yatalazimika kuingia katika kituo cha magari au eneo lolote ambalo limetengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo.

Utaratibu wa kutoza Ushuru

5.-(1) Halmashauri itatoza ushuru kwa kila basi, gari, pikipiki, teksi au chombo chochote cha usafiri kinachofanana na hivyo kitakachoingia na kitakachoegeshwa katika kituo cha magari au eneo lililotengwa kwa ajili ya kushushia abiria au maegesho kama ilivyoelekezwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mtu atakayelipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi atatakiwa kupewa risiti ya kielectroniki na atakayelipa ushuru atatakiwa kudai risiti.

(3) Mmiliki wa gari la abiria au mizigo anaposhindwa au kukataa kulipa ushuru, ushuru huo utakusanywa kwa njia ya mahakama ikiwa ni pamoja na kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Bila kuathiri kifungu cha 5(3), Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata chombo cha usafiri na kushikilia mpaka utaratibu wa kulipa ushuru huo utakapolipwa.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya ushuru au kwa gari lililokamatwa na kushikiliwa hii ikijumuisha pia mali zilizomo ndani ya gari husika, isipokuwa kama hasara iliyotokea itakuwa imesababiswa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

(6) Mtu yeyote atakayeingia katika kituo cha mabasi ambaye hatakuwa na tiketi atatakiwa kulipa ushuru wa shilingi 200.

(7) Halmashauri itakodisha eneo, jengo au kibanda kilichopo ndani ya kituo cha mabasi pamoja na maeneo mengine ya minada na masoko ambapo wakodishwaji watalazimika kulipa kodi ya eneo au pango ambapo mita moja ya mraba itakuwa shilingi 8000.

(8) Mabango yoyote yanayowekwa katika eneo lolote ndani ya kituo yatatakiwa kulipiwa ada ya eneo lililowekwa bango hilo kulingana na bei ya soko kwa wakati huo.

(9) Mawakala wote watakaokuwa wanahusika na kukata tiketi za abiria watatakiwa kujisajili Halmashauri na kulipa ushuru wa shilingi 1000 kwa siku.

Marufuku

6. Itakuwa ni marufuku kwa wapiga debe pamoja na wafanyabiashara ndogondogo (machinga) kuingia ndani ya kituo.

Huduma ya choo

7.-(1) Kutakuwa na huduma ya choo katika kituo cha magari au mabasi ambapo kila mtumiaji atatakiwa kulipa.

(2) Huduma ya haja ndogo na kubwa italipiwa shilingi (300) na huduma ya bafu itakuwa shilingi mia tano (500).

Usafi wa mazingira

8.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba vituo vyote vinabaki katika hali ya usafi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazohusiana na mambo ya Afya na Mazingira.

(2) Kila mmiliki wa gari atahakikisha anaweka chombo cha taka ndani ya gari lake na kutunza uchafu huo ili kuweka hali ya kituo katika mazingira mazuri, safi na yenye kuvutia.

(3) Haitaruhusiwa kwa abiria au mtu yeyote yule kutupa taka hovyo, kumwaga maji hovyo au kutiririsha maji, kuosha gari au chombo chochote cha usafiri ndani ya kituo cha magari.

Muda wa kufungua na kufugwa vituo

9. Vituo vyote vya magari vitafunguliwa saa kumi na moja alfajiri na kufungwa saa nne usiku.

Makosa

10. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashusha na kupakia abiria au mizigo katika eneo ambalo halikutengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo;

(b) atakataa au kujaribu kukataa kulipa ushuru;

(c) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ushuru;

(d) atachafua mazingira kwa namna yoyote ile;

(e) ataegesha gari lake katika eneo ambalo siyo rasmi au lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote viwili kwa pamoja faini na kifungo.

Sheria Ndogo Tangazo la Serikali Na. 190 la tarehe 10/10/2008 zinafutwa

12. Sheria Ndogo za (Kituo cha Mabasi) za Halmashauri ya Mji Kibaha za mwaka 2008, Gazeti la Serikali Namba 190 la tarehe 10/10/2008 zinafutwa.

Kufifilisha makosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini mkosaji isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) kwa mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa katika jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa chini ya kifungu cha 5(1)*

USHURU WA MAGARI YA ABIRIA NA MIZIGO

| *Na.* | *Aina ya Gari* | *Kiasi cha Ushuru* | *Muda* |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabasi Makubwa | 2000 | Kila linapoingia stendi |
| 2. | Mabasi ya Kati (Coaster) | 1000 | Kila linapoingia stendi |
| 3. | Magari Madogo (Hiace) | 500 | Kila linapoingia stendi |
| 4. | Taxi, Pick-Up, Kirikuu, Bajaji ikiegesha ndani ya kituo cha basi | 1000 | Kwa siku |
| 5. | Taxi, Pick-Up, Kirikuu, Bajaji ikiegesha nje ya kituo cha basi | 500 | Kwa siku |
| 6. | Pikipiki ikiegesha ndani ya kituo | 500 | Kwa siku |
| 7. | Pikipiki ikiegesha nje ya kituo | 300 | Kwa siku |
| 8. | Gari binafsi akiingia/akiegesha nje na ndani ya kituo | 300<br>500<br>1000 | - Kwa nusu saa<br>- Kwa saa<br>- Kwa siku |
| 9. | Taxi, Pick-Up, Kirikuu, Bajaji | 300 | Kila linapoingia ndani ya kituo cha magari kushusha abiria na kutoka. |
| 10. | Pikipiki | 200 | Kila linapoingia ndani ya kituo cha magari kushusha abiria na kutoka. |

JEDWALI LA PILI

---

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 13)*

Mimi ...................................................................... wa S. L. P. .......................... ninayeishi .................................... nakiri kuwa leo tarehe ..................... nilikiuka kifungu cha .......................... cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Mji Kibaha za mwaka 2018. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninachodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa madaraka aliyopewa Mkurugenzi chini ya kifungu cha Sheria Ndogo hizi.

Sahihi: .........................................................,

**MBEYE YANGU:**

JINA: ...........................................................................................

SAINI: .........................................................................................

WADHIFA: ...................................................................................